

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Barua pepe : [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.

*Dodoma  
24 Aprili, 2024*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**TANGAZENI MAPITO YA MUUNGANO KWA ZAWADI ZA VITABU - SAMIA**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameelekeza Viongozi pamoja na Watanzania kwa ujumla kugawa vitabu vinavyoeleza mapito ya Muungano kama zawadi kwa viongozi na wageni wa nchi za nje.

Rais Samia ametoa kauli hiyo leo wakati akizindua vitabu vya Miaka 60 ya Historia ya Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Kitabu cha Safari za Picha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka 60 kwenye hafla iliyofanyika Ikulu, Chamwino.

Aidha, Rais Samia amesema vitabu hivyo ni kumbukumbu muhimu kwa taifa na kwa Watanzania kwa kuwa watasoma na kupata taarifa mbalimbali ambazo hazipatikani kirahisi sehemu nyingine.

Rais Samia pia amesema vitabu hivyo vitawawezesha kukuza ujuzi na kujiongeza maarifa kuhusu Muungano wetu adimu na adhimu pamoja na kutunza historia inayoweza kutumika katika mambo kadhaa ikiwemo utalii.

Vile vile, Rais Samia amewasihi Watanzania kuendelea kudumisha amani, umoja na mshikamano wa Taifa letu, kufanya kazi kwa bidii na kudumisha uzalendo kwa kuenzi kwa vitendo Muungano na Waasisi wake.

Uzinduzi wa vitabu hivyo ni sehemu ya shamrashamra ya sherehe za Muungano ambapo awali Rais Samia aliwatunuku Nishani za Muungano viongozi mbalimbali waliopo madarakani pamoja na wastaafu.

A handwritten signature in blue ink.

Zuhura Yunus  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

